Grade 9 - Kiswahili Karatasi ya 1

Junior School Assessment

SEHEMU A: KUSOMA UFAHAMU (alama 25)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1-6

Ni furaha ya kila mzazi kuona watoto wake wakipata elimu ya kufana itakayowawezesha kufaulu katika maisha yao. Hivyo basi wao hutumia fedha nyingi kuwalipia karo katika shule nzuri ili waweze kunufaika kimasomo. Shule nyingi za kibinafsi na za serikali zimejaa kote katika juhudi za kukimu mahitaji ya idadi kubwa ya wanafunzi.

Elimu bandia imeanza kujipenyeza katika sekta hii muhimu. Utapata kuna baadhi ya watu ambao wanachukulia sekta hii kuwa ni biashara na mahali pa kujitajirisha kwa kasi. Wanaanzisha shule au taasisi za elimu bila kuzingatia na kufuatilia utaratibu uliowekwa. Hivi majuzi kumekuwa na tetesi ambapo baadhi ya shahada zitolewazo na chuo kimoja kikuu ziliharamishwa na serikali. Wazazi waliokuwa wametumia maelfu ya pesa kuwaelimisha wanao walizubaa wasijue la kufanya.

Moja kati ya majukumu ya elimu ni kuhakikisha kuwa wanafunzi watakuwa watu wa kutegemewa katika siku za usoni. Ingawa taasisi zetu za elimu zinatoa mafunzo kuhusu njia mwafaka za ukulima, ni kinaya kuona kwamba wananchi wetu bado wanapigana na tatizo la njaa. Hata wale wanaofuzu, wanapuuza na kuendelea na mitindo ya zamani ya ukulima na iliyopitwa na wakati. Hii inatokana na imani potovu kuwa elimu ni ya kupita mtihani wala sio kuwawezesha kufaulu katika maisha yao ya baadaye.

Ni aibu kubwa kuwaona wanafunzi wamefuzu kutoka vyuo vikuu lakini wapatiwapo kazi kama ya udaktari ama uhandisi wanalemewa kuifanya ama wanafanya kazi mbaya. Jambo kama hili husababisha matatizo makubwa kwa wale wanaowahudumia. Fikiria, kwa mfano, iwapo daktari atashindwa kufanya kazi yake, licha ya kufuzu vizuri, mgonjwa atapata afueni na suluhisho kutoka wapi?

Elimu inafaa kuwafunza watu adabu na kuwafanya wawe wa kutegemewa siku za usoni. Hata hivyo, si mara moja ambapo tumeshuhudia wanafunzi wetu wakiwa na tabia zisizotamanika baada ya kumaliza shule. Hii ndiyo sababu katika miji yetu utapata kuna makahaba, majangili na watumizi sugu wa dawa za kulevya waliosoma na hata kufuzu kutoka vyuo vikuu.

Maswali

1. Yape makala uliyoyasoma kichwa mwafaka.
   A. Elimu. B. Wizara ya elimu
   C. Changamoto katika sekta ya elimu. D. Umuhimu wa elimu maishani mwa binadamu.
2. Jambo ambalo linawafanya wazazi kuthamini elimu ni kuwa huwawezesha watoto wao
   A. kunufaika katika elimu
   B. kufaulu katika maisha yao
   C. kujua jinsi ya kuishi katika ulimwengu wa sasa
   D. kujua matatizo yanayowakumba.
3. Elimu bandia imejitokeza vipi katika sekta ya elimu?
   A. Kuchukua hongo ili kuwapa wanafunzi nafasi katika chuo.
   B. Serikali kuwasajili wanafunzi wachache shuleni.
   C. Kuanzisha taasisi za elimu bila kuzingatia utaratibu uliowekwa.
   D. Wanafunzi kujiingiza katika wizi wa mitihani.
4. Imani potovu ambayo hujitokeza kuhusu elimu kwa wanafunzi ni kuwa
   A. kuna baadhi ya shule ambazo zinawapa wanafunzi wao cheti bandia
   B. elimu ni ya kupita mtihani wala sio kuwawezesha kufaulu mtihani
   C. elimu inaweza kutolewa na walimu pekee shuleni
   D. elimu katika shule za kibinafsi ni bora kuliko shule za serikali.
5. Ni kinaya kipi kinachohusiana na suala la elimu kinajitokeza kutoka kwenye kifungu hiki?
   A. Kuwa elimu inatawaliwa katika baadhi ya taasisi tu.
   B. Kuwa baadhi ya shahada zitolewazo na chuo kikuu kimoja ziliharamishwa na serikali.
   C. Kuwa mwanafunzi asiyefuzu vizuri hatabarikiwa maishani mwake.
   D. Wananchi bado wanapigana na tatizo la njaa hata baada ya kupata elimu ya ...